Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.281
Volume: 03 Issue: 01 | Oct-2021|
Received: 01.10.2021; Accepted 04.10.2021; Published on 20.30. 2021 at www.editoncpublishing.org
Tibezuka B. C., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

# Mabadiliko Katika Uteuzi wa Majina ya Koo Miongoni mwa Wazinza Nchini Tanzania.

**Authors.**
**Tibezuka B. Clementina[1]; Lina Akaka[2]; Jane Maithya[3]**
**[1.2.3] Laikipia University, Kenya.**
**Main author email: tibezukamtaki@gmail.com**

## IKISIRI

Makala hii inachambua mabadiliko yaliyopo katika uteuzi wa majina ya koo miongoni mwa Wazinza na sababu zinazopelekea mabadiliko hayo katika utoaji wa majina kwa jamii ya Wazinza. Mila na desturi ni nguzo muhimu sana katika utamaduni wa jamii yoyote ile. Mila na desturi za jamii ni mambo ya kimsingi ya kuzingatia wakati wa kuteua majina, hata hivyo mila hizi zimepuuzwa kwa miaka ya hivi karibuni katika jamii ya Wazinza hivyo kupelekea kuwepo kwa mabadiliko makubwa katika uteuzi wa majina ya koo kwa kutofuata mila na desturi. Utafiti uliongozwa na nadharia ya Makutano na Mwachano iliyoasisiwa na Giles (1982). Mtafiti alitumia mihimili mitatu ya nadharia ya Makutano na Mwachano. Sampuli za utafiti ziliteuliwa kwa kutumia mbinu za kimaksudi na kuelekezwa. Watafitiwa kumi na nane wenye umri wa kati ya miaka 25-90 walichaguliwa. Ukusanyaji wa data uliongozwa na miongozo miwili ya maswali; mmoja wa mijadala ya vikundi lengwa na mwingine wa mahojiano ya kina. Baadhi ya mabadiliko haya ni kama vile; athari za utandawazi, elimu, dini, ndoa, tamaduni za kigeni, lugha za kigeni na watu mashuhuri katika jamii.

**Maneno muhimu:** Majina ya Koo, Mila na desturi, Utamaduni wa jamii.

---------------------------------------------------------------------***---------------------------------------------------------------------

**How to cite this article in APA.**

Tibezuka B. C., Akaka, L. & Maithya, J. (2021). Mabadiliko Katika Uteuzi wa Majina ya Koo Miongoni mwa Wazinza Nchini Tanzania. *Editon Cons. J. Kiswahili,* 3(1), 307-314. https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v3i1.281

---------------------------------------------------------------------***---------------------------------------------------------------------



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.281
Volume: 03 Issue: 01 | Oct-2021|
Received: 01.10.2021; Accepted 04.10.2021; Published on 20.30. 2021 at www.editoncpublishing.org
Tibezuka B. C., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

**UTANGULIZI**

Ni dhahiri kwamba majina ya koo yanatokana na mila na desturi za wanajamii husika kulingana na mazingira ya jamii husika. Majina hayo yanapotumika huwa yanaitambulisha jamii hiyo. Mila na desturi ni mfumo wa kikabila ambao huainisha na kutenganisha kila kitu, vituko na vijimambo vinavyotokea kwenye mazingira ya pamoja. Mila na destrui uainisha jamii, kiasi kwamba mawazo, matarajio na kanuni zao ni sawa (Wizara ya Elimu na Utamaduni Tanzania, 2005). Mabadiliko yanayoonekana sasa ni matokeo ya kutofuata mila na desturi katika uteuzi wa majina.

**Msingi wa Nadharia**

Utafiti uliongozwa na nadharia ya Makutano na Mwachano iliyoasisiwa na Giles (1982). Mihimili mikuu ya nadharia hii ambayo ni: muktadha wa kijamii, mwelekeo wa makazi, na matukio ya kijamii ulitumiwa kubaini nafasi ya mila na desturi katika uteuzi wa majina ya koo miongoni mwa Wazinza. Kwa mujibu wa (Giles and Smith, 1979), wanaeleza kuwa makutano katika jamiilugha humaanisha mchakato ambao watu hubadilisha mwelekeo wa semi katika mwingiliano ili zifanane zaidi na mifumo ya jamiilugha za watumiaji wa jamiilugha mpya. Ilihali pale ambapo jamii lugha inapoendeleza utambulisho wake kwa kutumia lugha yake bila kutegemea jamii lugha nyingine tunasema ni mwachano. Kipengele hiki cha mabadiliko katika uteuzi wa majina ya koo kinasimamiwa na mhimili wa muktadha wa kijamii. Mhimili huu umetumiwa na mtafiti kuelewa namna mila na desturi zilivyo na nafasi katika uteuzi wa majina kwa watu na kuonyesha mabadiliko yaliyopo katika uteuzi wa majina yamesababishwa na utandawazi, msukumo wa kidini, kurithi tamaduni za kigeni, na msukumo wa kielimu.

**Mbinu za Utafiti**

Watafiti walitumia mbinu za uteuzi wa kimaksudi na kuelekezwa kuteua sampuli ya watafitiwa 18 ambao wanashiriki katika uteuzi wa majina kwa watoto. Data za watafitiwa hawa zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya mahojiano na kundi lengwa la mjadala. Kati ya watafitiwa 18 walioteuliwa, watafitiwa kumi na sita (16) waliteuliwa kwa maelekezo huku watafitiwa wawili (2) waliteuliwa kimaksudi ili kutafitiwa. Mtafiti alitumia mbinu hizi ili kupata uthabiti wa matokeo ya utafiti aliokusudia kuufanya. Pia, alitumia mbinu hizi ili zimsaidie kukusanya data kwa haraka na kwa wingi na mwisho mbinu zimsaidie kuhakiki data iliyokusanywa.

**Matokeo ya Utafiti**

Katika kujibu swali la ni mambo gani yaliyochangia mabadiliko katika uteuzi wa majina katika jamii ya Wazinza? Zamani katika jamii ya Wazinza mila na desturi za makabila ndizo zilikuwa msingi mkubwa wa aina ya majina waliyopatiwa watu, siku hizi hali imekuwa tofauti. Inaelezwa kuwa, hali ni tofauti siku hizi hasa kutokana na mabadiliko kadha wa kadha katika jamii ikiwemo; kuwepo kwa utandawazi, msukumo wa dini, kuiga tamaduni za kigeni, misukumo ya kielimu, ndoa, watu maarufu, pamoja na athari za lugha za kigeni.

**Mabadiliko Katika Uteuzi wa Majina Ya Jamii ya Wazinza**

Mabadiliko katika uteuzi wa majina yanaendana na vigezo katika uteuzi wa majina. Jamii nyingi ulimwenguni zinashuhudia mabadiliko katika uteuzi wa majina. Kwa mujibu wa Fischer (1986), huko Ulaya katika karne ya kumi na nane na kumi na tisa, kulishuhudiwa mabadiliko kwa kasi katika uteuzi wa majina. Anaeleza kuwa wazazi wengi huko Concord, Massachusetts waliwapa mmoja wa watoto wao jina lao la kwanza au jina la kibiblia; lakini badae tamaduni hii ilipungua sana. Matumizi ya majina ya babu na bibi kwa watoto yalipungua.

Fischer anaendela kusisitiza kuwa, pamoja na kupungua kwa majina ya kifamilia, uteuzi wa majina ulikuwa huru kuendeshwa na maadili ya kitamaduni na kidini. Kutokana na mabadiliko haya, majina mengi ya watoto yalionyesha



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.281
Volume: 03 Issue: 01 | Oct-2021|
Received: 01.10.2021; Accepted 04.10.2021; Published on 20.30. 2021 at www.editoncpublishing.org
Tibezuka B. C., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

kuwa na ushawishi wa kidunia, mfano, wazazi waliwapa watoto majina ya mashujaa wa vita, wanasiasa, na ata wafalme na malkia.

Naye Mahome (1972) katika utafiti wake kuhusu majina katika jamii ya Niitsitapi, kwa kutumia nadharia ya utambulisho wa jamii na mbinu za hojaji na mahojiano alieleza kwamba katika jamii za Niitsitapi barani Asia, majina yatolewayo huelezea historia ya watu ambayo yanapaswa kukumbukwa na kurithishwa katika kizazi kimoja hadi kizazi kingine. Hivyo, majina ya watoto yanayotolewa kwa kutumia upande wa baba au mama hudumisha majina ya wahenga wao.

Katika jamii hiyo ya Niitsitapi wanaamini kuwa, watoto wanaopewa majina hayo hutazamiwa kurithi tabia na matendo ya babu au bibi zao. Hata hivyo, utafiti huo ni tofauti sana na utafiti wetu kwani utafiti huo ulijikita sana kuchunguza dhima za majina ya watu katika jamii za Niitsitapi ili hali utafiti huu unalenga kuchunguza na kuelewa nafasi ya mila na desturi katika uteuzi wa majina ya koo katika jamii ya Wazinza.

Mabadiliko katika uteuzi wa majina ni matokeo ya athari za kijamii ambazo zimeonekana kuathiri watu waliobeba majina hayo. Jina analopewa mtoto linaweza kuwa na athari kubwa kwa mtoto akiwa mdogo na athari hiyo inaweza kujitokeza tena akiwa mtu mzima, kama tafiti zinavyo onyesha. Lusekelo (2018), akitafiti kuhusumajina yanavyo onyesha uhusiano ndani ya familia na kati ya koo kati ya Wanyakyusa, alibaini kuwa majina binafsi yamegawanywa katika majina ya kiume na majina ya kike ambapo mengi yanaakisi athari zilizowahi kutokea kijamii.

Mfano, mtoto wa kike aliyepewa jina la asili la bibi yake ambaye alikuwa na tabia ya uchawi au wizi mara nyingi imeonekana mtoto huyo alirithi tabia ya bibi yake hivo kuepelekea athari ya kutengwa na jamii au kuishi kwa hofu kutokana na tabia yake. Hii ilipelekea wazazi kuacha utamaduni wa kuwapa watoto wao majina ya asili ambayo hayakuwa na taswila nzuri. Hivyo, utamaduni wa kurithisha majina na wazee yanapotea polepole.

Katika kutafiti juu ya majina, mtafiti Jahoda (1954), alichunguza uhusiano wa majina na tabia za watu wa Ashanti katika Afrika ambapo aligundua kuwa siku aliyozaliwa mtu ilichangia katika mwonekano wa tabia yake maishani. Mfano, mtu aliyezaliwa siku ya msiba akapewa jina linaloashiria hali ya huzuni basi aliishi kwa huzuni maishani mwake. Hii imepelekea wazazi kuachilia mbali uteuzi wa majina kufuatia matukio ya kijamii ambayo yaliashiria tamaduni zenye huzuni na kutumia majina ya kisasa ambayo hayaashirii tamaduni zenye huzuni.

Guma (2001) alitafiti majina ya watu katika jamii ya Basotho huko Afrika ya kusini. Katika utafiti wake alibaini kuwa jina ni zaidi ya neno au maneno yanayomtambulisha mtu. Aliendelea kusema kuwa utoaji wa majina ni tukio la kijamii na kiutamaduni linaloonyesha historia ya jamii. Anaendelea kusema kuwa mabadiliko yanayoonekana sasa katika uteuzi wa majina ni matokeo ya msukumo wa kitaaluma katika jamii ambapo wazazi wengi walioelimika wameacha kuteua majina asilia yaliyomtambulisha mtu kulingana na histioria ya jamii yake bali wanateua majina kutokana na historia ya jamii ya wataaluma waliofanikiwa kimaisha. Mfano, jina Isaac Newton.

Mduma (2014) katika Makala yake ya 'Utamaduni wa kurithishana watoto majina unapotea' alimuhoji Sheikh Zuberi Kusagawa wa Dar es Salaam akaeleza mtazamo kuhusu majina: "Kiukweli inauma sana na kustaajabisha pale unapoona wazazi wanatoa majina kwa ushabiki na fashion [mitindo], huku Allah [Mungu] akiwa ametuagiza vyema kuwapa majina mazuri wanetu na yenye kumpendeza yeye Allah. Kwani hata mtu akijua vyema maana ya jina hilo itasaidia wanetu kuwa na nyendo zinazokubalika".



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.281
Volume: 03 Issue: 01 | Oct-2021|
Received: 01.10.2021; Accepted 04.10.2021; Published on 20.30. 2021 at www.editoncpublishing.org
Tibezuka B. C., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Kwa upande wake, Mpute (2016), mkazi wa Mwenge, Dar es Salaam anaeleza kuwa binafsi anaona kuwa wazee wa kale walikuwa sahihi walipokuwa wakiwapatia watoto majina yenye kuakisi mila na tamaduni kwani majina hayo yalibeba utu ndani yake pamoja na utambulisho wa mtu mmoja mmoja katika jamii. Majina haya yaliweka na kutunza heshima ya ukoo fulani kutokana na mienendo yao, pia yaliepusha kadhia ya ndugu kuoleana kutokana na kutokujua asili na utambulisho wao, tofauti na tunavyo shuhudia siku hizi.

Mukasa (2016), wa Dar es Salaam alieleza kuwa ndani ya miaka michache ijayo anategemea kuwa mama na angependa kuwapa wanae majina yanayosikika vizuri masikioni mwa watu bila kujali uasili au ugeni wake ila tu mvuto wake na hii itamfanya mtoto alifurahie jina lake. Wataalamu wa Saikolojia pia wanasema ni vyema jamii ikatambua kuwa jina ni mali, na suala hili la kuiga kila kitu hadi majina limechagizwa na utandawazi na kuna haja ya jamii kuzinduka na kupigania tamaduni zake.

Kwa mfano, Mbata (2011), Mwanasaikolojia na mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam anasema ameishi sana Italia na huko watu wanathamini mno majina yao lakini kwa Afrika mathalani Tanzania hili bado ni tatizo. Aidha, Mbata (ameshatajwa) anafafanua kuwa, kisaikolojia jina humfanya mtu ajione sehemu ya jamii husika kutokana na jina la mtu mmoja mmoja kuwa na uhusiano na majina ya wanajamii wenzake. Hii husaidia kuleta mshikamano, utu na hali ya undugu kwa familia na jamii kwa ujumla.

Kwa muktadha huu, ni vyema mzazi au mlezi na jamii husika kutafakari jina la kumpatia mtoto kwa kuzingatia mahitaji, mila na nyakati. Pia, ni muhimu kuzingatia ni kwa kiasi gani jina hilo litamuunganisha au kumtenga mhusika na jamii inayomzunguka, huku ukitathmini uzoefu wako na jina ulilonalo wewe mwenyewe.

Kwa sasa tunashuhudia wazazi wengi walioenda shule huwapa watoto wao majina kama vile; Newton, Dalton, Socrates, Ngugi, Okonko, Takadini na majina mengi ya watu waliofanya vyema katika nyaja za elimu na uvumbuzi. Mwemezi (2016), katika makala yake ya 'Majina ya kizazi kipya' anaeleza kuwa mzazi mmoja aliyefanikiwa kusoma hadi kidato cha nne na alipenda masomo ya Sayansi, alimpatia mwane wa kiume jina Newton ili kuenzi jina la mwana Fizikia nguli na mvumbuzi wa mambo mengi katika nyanja ya sayansi duniani.

Hii inatoa picha kwamba katika jamii zilizo nyingi wazazi waliopata elimu kiwango fulani huwapa watoto wao majina yanayoendana na majina ya watu waliofanya vyema katika nyanja za elimu. Hapa mtafiti atawekeza nguvu zaidi kutaka kujua taratibu zikoje kwa jamii ya Wazinza husussani kigezo cha kuwapa watoto majina ya kisasa kwa kuzingatia majina ya watu waliofanya mambo makubwa katika nyanja ya elimu. Hii ni kutokana na ukweli kuwa majina mengi ya kisasa (majina ambayo hayana asili ya kikabila) yanatokana na msukumo wa kielimu ambao wazazi wanakuwa nao hivyo kupelekea wao kuwapa watoto wao majina ya watu hao waliofanya vizuri katika elimu.

**Utandawazi**

Mojawapo wa mambo yalioathiri mabadiliko katika uteuzi wa majina ni utandawazi. Utandawazi ni mabadiliko katika mfumo wa kimataifa unaorahisisha mawasiliano na mahusiano katika sekta za kiuchumi, kibiashara, kisiasa, kielimu na kitamaduni uliojikita katika teknohama. Utandawazi umesababisha kwa kiasi kikubwa aina mpya ya uteuzi wa majina katika jamii ya Wazinza. Kwa mfano, mtoto kupatiwa jina la nyota wa kandanda, filamu, muziki, ndondi na hata michezo ya kikapu au majina ya viongozi maarufu katika nyanja mbalimbali kama vile siasa, uchumi na kadhalika hapa duniani. Pamoja na kwamba sio vibaya wazazi au walezi kuwapatia watoto



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.281
ISSN: 2663-9289
Volume: 03 Issue: 01 | Oct-2021|
Received: 01.10.2021; Accepted 04.10.2021; Published on 20.30. 2021 at www.editoncpublishing.org
Tibezuka B. C., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

wao majina hayo, kwani mojawapo ya sababu inayotajwa kusababisha kufanya hivyo ni wazazi kutamani watoto wao hapo baadaye kuwa kama hao wenye majina hayo au kuwataka waige na kufuata nyayo za mafanikio ya hao watu.

Lakini tatizo linakuja pale mtoa jina husika hafahamu asili na maana ya jina hilo; au kutofahamu haswa wazazi wa nyota au kiongozi huyo waliamua kumpa mtoto wao jina hilo na walikuwa katika hali gani. Kwa Mfano, baadhi ya wazazi waliwapa watoto wao jina *Magufuli* ambaye alikuwa mtu mashuhuri na maarufu wakiamini mtoto wao pia atakua katika maadili ya kiuongozi bila kujua kwamba uongozi ni kipawa kutoka kwa muumba wetu na viongozi huandaliwa ili kuwa na utendaji kazi ulio mzuri.

**Msukumo wa Dini**

Pamoja na utandawazi kuchangia pakubwa katika mabadiliko kwenye uteuzi wa majina miongoni mwa Wazinza, dini pia imekuwa njia mojawapo mahususi ya utoaji wa majina, kama ilivyo mila na desturi za mahali. Licha ya kuwa mfumo wa imani za dini katika jamii zipo tofauti, lakini imekua chanzo kikubwa cha uteuzi wa majina kwa baadhi ya watu, hasa katika jamii za Wazinza. Ni kwa sababu hii ya dini, yapo majina fulani (mfano; Hamisi, Juma na Janeth) mtu akiyasikia katika jamii hutosha kumtambulisha mwenye jina kuwa ni mfuasi wa dini fulani mfano Mkristo, Muislamu, na kadhalika. Hali hii imepelekea kuwepo na mabadiliko makubwa katika uteuzi wa majina miongoni mwa Wazinza hasa kuacha kutumia majina ya asili na kuanza kutimia majina yatolewayo Kanisani na Msikitini.

Mtafitiwa mmoja alieleza kupotea kwa utamaduni wa kurithisha watoto majina ya koo, alieleza kuwa: hakika inasikitisha pale wazazi wanapotoa majina kwa ushabiki na kufuata mitindo ya kisasa, ili hali Mungu alituagiza vyema kuwapa majina mazuri wanetu na yenye kumpendeza yeye. Kwani mtu akifahamu vyema maana ya jina hilo itasaidia pia watoto kuwa na tabia zinazokubalika. Alifafanua zaidi kuwa utoaji huu wa majina katika dini zote hulenga kuwafanya waumini kufuata njia sahihi pamoja na kujihisi sehemu ya dini husika.

Kwa upande mwingine, Mzee mmoja alieleza kuwa; binafsi anaona kuwa wazee wa zamani walikuwa sahihi walipokuwa wakiwapa watoto majina yenye kuakisi mila na tamaduni kwani majina hayo yalibeba utu ndani yake pamoja na utambulisho wa mtu mmoja mmoja katika jamii. Aliongeza kuwa, majina hayo yaliweka na kutunza heshima ya ukoo fulani kutokana na mienendo yao, pia yaliepusha kadhia ya ndugu kuoleana kutokana na kutokujua asili na utambulisho wao, tofauti na tunavyo shuhudia siku hizi.

**Kuiga Tamaduni za Kigeni**

Nje ya msukumo wa kidini kama chanzo cha mabadiliko kwenye uteuzi wa majina, zipo sababu nyingine za watu kupenda kutumia majina ya watu wa tamaduni za nchi nyingine duniani. Mtafitiwa mmoja anaeleza kuwa, mara nyingi watu huchukia majina yao ya asili na kupenda majina ya kizungu kutokana na mtazamo waliojiwekea kutokana na maana ya jina kwani hata yeye akiwa shuleni hakulipenda jina lake kwa sababu wanafunzi wenzake walimtania sana.

Ni dhahiri kuwa moja ya sababu za kuacha kutumia majina ya asili na kutumia majina ya kigeni ni uwepo wa majina ya asili ambayo maana yake ina tafsiri mbaya miongoni mwa wanajamii, hii inapelekea wazazi kupenda kuwapa watoto wao majina yanayosikika vizuri masikioni mwa watu bila kujali uasili au ugeni wake. Zaidi wanaangalia mvuto wa jina hilo na hii inamfanya mtoto alifurahie jina lake. Hivyo, ni vyema jamii ikatambua kuwa jina ni mali, vilevile kuna haja ya wazazi kuteua majina yanayoakisi uzuri na kupigania tamaduni za jamii yake.



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

ISSN: 2663-9289
DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.281
Volume: 03 Issue: 01 | Oct-2021|
Received: 01.10.2021; Accepted 04.10.2021; Published on 20.30. 2021 at www.editoncpublishing.org
Tibezuka B. C., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Aidha, jina humfanya mtu ajione sehemu ya jamii husika kutokana na jina la mtu mmoja mmoja kuwa na uhusiano na majina ya wanajamii wenzake. Hii husaidia kuleta mshikamano, utu na hali ya undugu kwa familia na jamii kwa ujumla. Kwa muktadha huu, ni vyema mzazi au mlezi na jamii husika kutafakari jina la kumpatia mtoto kwa kuzingatia mahitaji, mila na nyakati. Pia, ni muhimu kuzingatia ni kwa kiasi gani jina hilo litamuunganisha au kumtenga mhusika na jamii inayomzunguka. Hivyo, kuna mabadiliko ya wazi katika uteuzi wa majina mfano; kuacha kuteua majina kama vile tabu, shida ambayo hayasiikiki vyema masikioni mwa watu na kuanza kuteua majina kama vile Faraja, Baraka na Imani ambayo yanasikika vyema masikioni mwa watu.

**Msukumo wa Kielimu**

Kukua kwa misingi ya elimu na matokeo chanya ya elimu katika jamii ni moja ya misukumo inayopelekea mabadiliko kwenye uteuzi wa majina ya kuwapa watoto katika jamii ya Wazinza na jamii zilizo nyingi kwa ujumla. Katika kipengele hiki, mtafiti alibaini kuwa katika jamii ya Wazinza kuna majina gani wamepewa watoto ambayo yametokana na msukumo wa kielimu kwa wanajamii. Wazazi wengi wamewapa watoto wao majina ya watu mashuhuri katika nyanja ya elimu ambapo baadhi ya watu hao mashuhuri walikwisha kuaga dunia au wako hai.

Kwa sasa inadhihirika wazi kuwa wazazi wengi walioenda shule wanawapa watoto wao majina kama vile; Newton, Dalton, Socrates, Okonko, Takadini na majina mengi ya watu waliofanya vizuri katika nyaja za elimu na uvumbuzi. Mtafitiwa mmoja ambaye ni mzazi na alifanikiwa kusoma hadi kidato cha nne na alipenda masomo ya Sayansi, alimpatia mwane wa kiume jina Newton ili kuenzi jina la mwana Fizikia nguli na mvumbuzi wa mambo mengi katika nyanja ya sayansi duniani. Anaeleza kuwa alimpatia jina hilo kwa sababu anapenda sana Fizikia.

Hii inatoa picha kwamba, ata katika jamii zilizo nyingi nje na Wazinza wazazi waliopata elimu kiwango fulani huwapa watoto wao majina yanayoendana na majina ya watu waliofanya vizuri katika nyanja za elimu. Hapa mtafiti aliweza kujua taratibu za uteuzi wa majina kwa jamii ya Wazinza hususani kigezo cha kuwapa watoto majina ya kisasa kwa kuzingatia majina ya watu waliofanya mambo makubwa katika nyanja ya elimu. Asilima kubwa ya majina ya kisasa (majina ambayo hayana asili ya kikabila) yanaoneka kutokana na msukumo wa kielimu ambao wazazi wanakuwa nao hivyo kupelekea wao kuwapa watoto majina ya watu hao waliofanya vizuri katika nyanja ya elimu wakiamini pia watoto wao watafanya vizuri.

**Msukumo wa Ndoa**

Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu, muingiliano wa kikabila wakati wa ndoa, kwa maana ya kwamba mtu wa kabila moja kuolewa na mtu wa kabila jingine tofauti ni jambo linalosababisha watu kuacha mila na desturi za kuwapa watoto majina kwa kufuata tamaduni za kabila husika. Mtafiti alibaini kwamba si wazazi wote wanafuata matakwa ya tamaduni za makabila yao katika uteuzi wa majina kwa watoto. Mtatifi alibaini wazi kuwa sababu zinazopeleka hali hii ya kutoteua majina asilia katika jamii ya Wazinza ni mwingiliano wa kikabila kwa wanandoa.

Mtafitiwa mmoja alisema kwamba, utamaduni wa kurithisha majina ya ukoo kwa watoto unapotea kwa sasa. Kati ya watafitiwa 18 waliohojiwa ili kutaka kujua kama wanafuata mila za makabila yao katika kurithishana majina ya ukoo kwa watoto, watafitiwa nane walisema wanafuata mila na desturi za makabila yao na zina umuhimu wake. Lakini watafitiwa kumi walisema kwa sababu walikulia katika familia za kidini nje ya wilaya ya Buchosa hawakupata fursa ya kuzijua mila na desturi za Kizinza.



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.281
Volume: 03 Issue: 01 | Oct-2021|
Received: 01.10.2021; Accepted 04.10.2021; Published on 20.30. 2021 at www.editoncpublishing.org
Tibezuka B. C., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Watafitiwa hao walipoulizwa endapo wakipata watoto katika ndoa zao watawapa majina ya wazazi wao, walijibu kwa kusema kuwa endapo watapata watoto wa kiume watawapa majina ya baba zao na watoto wa kike watawapatia majina ya mama zao. Wahojiwa hao walieleza zaidi kwamba: majina hayo hayana maana yoyote kidini au kimila, isipokuwa ni imani yao kwamba kuwapa watoto majina ya wazazi ni ishara ya upendo na heshima kwa wazazi wao. Mtafitiwa mwingine mwenye mtoto mmoja wa kike aitwaye Elizabeth katika ndoa yake, anaeleza kuwa haamini katika kuwarithisha watoto majina ya babu au bibi zako kwa sababu mbalimbali, kubwa ikiwa kuepuka kuwarithisha tabia za bibi au babu zako kama vile; ulevi, uchawi, wizi, umalaya, uongo na tabia nyingine nyingi zisizompendeza Mungu.

**Msukumo wa Watu Maarufu**

Moja ya misukumo inayopelekea mabadiliko ya uteuzi wa majina ya koo miongoni mwa Wazinza na jamii zilizo nyingi kwa ujumla ni ushawishi wa watu maarufu katika jamii zetu. Katika kipengele hiki, mtafiti alibaini kuwa katika jamii ya Wazinza kuna majina mengi ambayo yametokana na msukumo wa watu maarufu. Wazazi wengi huwapa watoto wao majina ya viongozi mashuhuri waliokwisha kuaga dunia au walio hai. Jambo hili ni ishara kuwa jamii zilizo nyingi zinahusudu sifa na hulka za viongozi hao. Aidha umaarufu hutokana na sifa za uongozi katika nyanja mbalimbali kama vile siasa, michezo, mitindo na mapishi.

Mfano hai nje ya jamii ya Wazinza ni kabila la Wajaluo nchini Kenya ambalo linajulikana kwa kuwapatia watoto wao majina ya watu maarufu. Baadhi ya akina mama kutoka jamii ya Wajaluo waliwapa watoto wao wavulana jina la Obama mwaka 2008 baada ya rais huyo wa Marekani mwenye asili ya Kijaluo kuchaguliwa kuwa rais. Majina ya Churchill na Clinton ni majina maarufu sana katika maeneo ya kabila la Waluo.

Miongoni mwa Wazinza, mfano mwaka 2015 kuna mzazi mmoja aliyempatia mwanae jina la 'Pombe Magufuli'. Mzazi wake alikaririwa akisema kuwa waliamua kumuita mtoto wao jina hilo kwa sababu walipendelea sana sera za Rais huyo mteuli hasa hasa falsafa yake ya 'Hapa kazi Tu!'. Hivyo kwa kiwango kikubwa sasa kutoa majina kwa watoto kulingana na majina ya watu maarufu katika jamii mbalimbali sio jambo geni tena. Hivyo, msukumo wa watu maarufu umepekelea wazazi wengi miongoni mwa jamii ya Wazinza kuwapa watoto wao majina kulingana na majina ya watu maarufu.

**Athari za Lugha za Kigeni**

Lugha za kigeni kama vile kiingereza ni moja ya misukumo inayopelekea mabadiliko yaliyopo katika uteuzi wa majina ya watoto kwenye jamii ya Wazinza na jamii zilizo nyingi kwa ujumla. Katika kipengele hiki, mtafiti alibaini kuwa katika jamii ya Wazinza kuna uteuzi wa majina ya watoto ambayo yametokana na athari za lugha za kigeni. Wazazi wengi katika nyakati hizi huwapa watoto wao majina kama vile Peace (Amani), Gift (Zawadi), Loveness (Pendo) na mengine mengi ya asili hiyo ikiwa ni majina yaliyotafsiirwa kutoka Kiswahili kwenda kiingereza. Hii ni ishara ya wazi kuwa jamii zilizo nyingi zinawapa watoto majina ya Kiingereza ambayo msingi wake ni Kiswahili.

**Mahitimisho na Mapendekezo**

Kwa kuwa utafiti huu ulichunguza mabadiliko yaliyopo katika uteuzi wa majina ya koo miongoni mwa Wazinza kwa kutimia nadharia ya Makutano na mwachano ambayo hutazama historia ya wanajamiilugha, mienendo yao, tamaduni zao na hata mila zao, kitu kipya tulichokibaini katika utafiti huu ni kuwa, maadili, mwenendo na maendeleo ya mtanzania kisiasa, kiuchumi, kijamii na hata kiutamaduni sasa na siku zijazo yataendelea kuporomoka kwa sababu misingi ya vitu vyote hivi umejengwa kupitia msingi wa utamaduni anamoishi mtu huyo kitu ambacho vinaonekana kuachwa na kupuuzwa kwa kasi na watu wengi.



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.281
Volume: 03 Issue: 01 | Oct-2021|
Received: 01.10.2021; Accepted 04.10.2021; Published on 20.30. 2021 at www.editoncpublishing.org
Tibezuka B. C., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Jambo jingine lililobainika katika utafiti huu ni kuwa, uteuzi wa majina ya koo kwa watu hivi sasa hauzingatii vigezo, taratibu na kanuni zilizobeba maana kulingana na utamaduni, mila, desturi na imani ya jamii husika. Hivyo, nafasi ya mila na desturi katika uteuzi wa majina ya koo imepuuzwa, kumbe kuna sababu za kurejea kwenye mila na desturi za uteui wa majina ya koo kwa watu kwani majina ya watu ambayo hubebwa na lugha ya watu husika katika jamii yoyote ile ndiyo yanayobeba na kutambulisha jamii hiyo kisiasa, kiuchumi kijamii na kiutamaduni kuliko vitu vingine kwani jina la mtu linabeba na kuakisi utamaduni, mila, desturi, falsafa na imani ya mtu huyo.

Kwa kuwa Kizinza ni miongoni mwa lahaja katika lugha ya Kisukuma, waandishi wanapendekeza kuwa kuna haja ya kufanya utafiti katika lahaja zingine za kisukuma ili kusaidia kuongeza machapisho katika lugha ya Kisukuma. Na kwa vile imekuwa vigumu kuweza kushughulikia kila kitu kilichohusiana na majina katika jamii ya Wazinza, vipo vipengele vingine vya kiisimu ambavyo vipo nje ya mawanda ya utafiti huu ambavyo pia havina budi kufanyiwa Uchunguzi. Hivyo, tafiti nyingine zinaweza kufanywa kuhusu vipengele vingine vya kiisimu katika lugha ya Kizinza, kwa mfano fonolojia ya lugha ya Kizinza, mofolojia ya lugha ya Kizinza, na vipengele mbalimbali vya kisintaksia katika lugha ya Kizinza. Vipengele hivi vikifanyiwa utafiti wa kina vitaweza kutoa mchango katika kubainisha lugha ya Kizinza.

## MAREJELEO

Fischer, D. H. (1986). "Forenames and the Family in New England: An Exercise in Historical Onomastics." in *Generations and Change*, edited by R. M. Taylor.

Giles, H., & Smith, D. (1979). "An intergroup Approach to Second Language Acquasition", *Journal of Multilingual and Multicultural Development* 3(17)-40 – 57.

Giles, H., (1982). "An intergroup Approach to Second Language Acquasition", *Journal of Multilingual and Multicultural Development* 3(17), 40 – 57.

Guma, M. (2001). The Cultural Meaning of Names among Basotho of Southern Africa. *Nordic Journal of Africa Studies* 10(3), 265 – 279.

Jahoda, G. (1954). "A Note of Ashanti Names and Their Relationship to Personality". *British Journal of Psychology* 45 (1954), 192-195. http://www.behindthename.comlarticiesll.php.

Lusekelo, S. (2018). *Traditional African Names*. http://www.namesite.coml Accessed 07/09/2021.

Mahome, A. (1972). *The Social and Literary Aspect of Zulu Perso Names*. Unpublished M.A Dissertation, University of Natal.

Mbata, L. (2011). *Maana na Misingi ya Uteuzi wa Majina ya Watu katika Lugha ya Kiha*. Tasnifu ya M.A Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Hajachapishwa).

Mwemezi, N. (2016). 'Majina ya kizazi kipya.' https://www.ippmedia.com/sw/makala/

Namsembaeli, M. (2014). 'Utamaduni wa kurithisha watoto majina Unapotea.' https://www.ippmedia.com/sw/makala/

Smith, D. S. (1984). "Child-Naming Practices as Cultural and Familial Indicators." in *Local Population Stduies* 32 (spring).



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org